JINA: ................................................ NAMBARI: ....................................

SHULE: ............................................ TAREHE: ........................................

SAHIHI:...........................................

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA PILI

MUDA: SAA 2½

# JARIBIO LA MTIHANI WA MWAKA - 2016

## KIDATO CHA PILI

**Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA PILI**
**MUDA: 2½**

**MAAGIZO**

1. Andika **jina lako** na **nambari yako** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. **Tia sahihi** yako kisha **uandike tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali **yote**.
4. Majibu **yote** yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
5. Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
6. *Usitoe* ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
7. **Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
8. **Watahaniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

| SWALI | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| Ufahamu | 20 | |
| Matumizi ya lugha | 40 | |
| Isimu Jamii | 10 | |
| Fasihi | 10 | |
| JUMLA | 80 | |



for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**UFAHAMU (ALAMA 20)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Kingi alizaliwa Vuruni, kijiji kilichosifika kwa ukarimu wa wanakijiji wake. Ingawa walikuwa karimu, Wavuruni wengi walikosa elimu. **Fauka ya** hayo, walining'inia katika umaskini uliokithiri. Hivyo wengi waliselea katika kazi za kijungu jiko. Watoto wa umri wa kwenda shule walikosa elimu na kuzurura mitaani. Udhaifu huu ulimpa faida Mwakisu, tajiri mmoja aliyemiliki shamba kubwa. Aliwaajiri watoto hao.

Mwakisu alikuwa **mkwasi** aliyetononoka si haba. Kama ni senti, alikuwa nazo. Kilichotia doa jina lake ni kiburi. Mbali na kiburi hicho, yeye hakujaliwa moyo wa huruma na utu. Hakubarikiwa kuwa mwema. Maadili hutuongoza kila mara kuwa 'wema hauozi.'

Kwa Mwakisu, wema ulioza na **kuvunda.** Utu uling'oka katika bawaba za moyo wake na ukawa msamiati aliouchukia. Aliwatumikisha watoto wa wenzake huku wake wakisoma shule. Tabia yake hiyo ndiyo iliyowafanya Wavuruni kumtoa katika orodha yao ya watu wema.

Mwakisu alistaajabisha! Hakutaka kununua mashine zozote za kufanya kazi shambani ingawa alikuwa na uwezo. **Alistahabu** kuajiri watoto wadogo na kuwadhulumu. Mkwasi huyu alifurahia kuona vitoto vikimenyana na kazi shambani kwake tangu mawio hadi machweo na hatimaye kuwapa ujira mdogo.

Siku moja Kingi alimtaka radhi, "Bosi naomba uniongezee chochote, kwani tuna shida nyumbani." Mwasiku alimkodolea macho huku mdomo ukimcheza. Hapo alimchomolea mwajiriwa wake tusi kubwa kutoka kwenye hazina yake isiyopungua. Tusi ambalo lilimtaabisha Kingi kulisahau. Lilikaririwa akilini mwake kwa sonono. Tangu siku hiyo Kingi akaona kuwa kuajiriwa na Mwakisu ni kufadhiliwa, na uso wa kufadhiliwa u chini.

Kiburi cha Mwakisu kilidhihirika kila mara. Kila alipomwona mtoto akilia kwa uchovu au maumivu, ungemsikia akimfokea, "Chapa kazi! Unalilia nani hapa? Kama humudu kazi rudi kwa mamako ukanyonye."

Kazi nyingi zilikuwa ngumu na hazikuwastahili watoto wenye umri mdogo. Si kipupwe, si kaskazi, si vuli, si kiangazi, si kusi; kazi ziliongezeka na kuwaumiza watoto. Kingi, kwa mfano, alitakikana akame ng'ombe kumi na abebe maziwa hadi kwenye tangi kubwa. Kisha angewakatia ng'ombe nyasi na kuwasafisha. Hatimaye angehitajika kuzoa samadi.

Msimu wa kipupwe uliwadia. Baridi ikawatafuna watoto hao waliokosa mavazi bora. Kingi aliugua. Watoto wengi wakapatwa na maradhi. Wawili wakaaga dunia. Wazazi walipoona maisha ya watoto wao yamo hatarini, wakaandamana hadi kwa Mwakisu. Tajiri huyo aliwajia kwa meno juu, "Msinitie kibuhuti. Mimi niliwaajiri watoto, sio watoto na wazazi wao." Wazazi wakatanabahi kuwa, 'Pa shoka hapaingii kisu.' Waliandamana hadi kwa chifu. Chifu alipoyaona yamempita kimo, akafululiza hadi kituo cha polisi.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Mwakisu akakamatwa, akashtakiwa na kuhukumiwa. Alipatikana na makosa ya kuwaajiri watoto wenye umri mdogo na kusababisha vifo vya wawili wao.

Serikali ikatoa amri kwa wazazi kupeleka watoto wao shuleni. Ikatoa pia misaada ya kuendeleza elimu; elimu ya bure kwa shule za msingi. Kingi akasoma hadi kuhitimu chuo kikuu. Akawa daktari.

Alfajiri moja mahabusi waliletwa hospitali kuu ya mkoa kwa matibabu. Kingi akampa huduma mzee aliyejawa mvi na **kukoboka** meno. Alipomtazama kwa makini akamkumbuka. Mwakisu akabahatisha, "Sura yako ...ni kama Kingi..." Kingi akamjibu, "Mimi ndiye Kingi. "Wakakodoleana macho, huku machozi yakimtiririka Mwakisu.

**Maswali**

(a) Taja matatizo **mawili** yaliyowakability wanakijiji cha Vuruni. (alama 4)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(b) Ni mambo gani yaliyowafanya wanakijiji kumtoa Mwakisu katika orodha yao? (alama 2)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(c) Mwakisu alishtakiwa kwa makosa gani? (alama 2)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(d) Eleza maana ya sehimi hizi: (alama 8)

(i) Kazi ya kijungu jiko:..........................................................................

..........................................................................................................

(ii) Tononoka si haba:..........................................................................

..........................................................................................................

(iii) Kodolea macho:..........................................................................

..........................................................................................................

(iv) Chapa kazi:..........................................................................

..........................................................................................................

(e) Toa maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika makala. (alama 4)

(i) Fauka ya:..........................................................................

..........................................................................................................

(ii) Mkwasi:..........................................................................

..........................................................................................................



for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

2. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

1)

(a) Taja aina **mbili** kuu za sauti tulizo nazo. (alama 2)

(i) ..............................................................................................................

(ii) ..............................................................................................................

(b) Eleza sifa kuu za irabu za Kiswahili. (alama 2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(c) Fafanua sifa za sauti zifuatazo za konsonanti na kwa kila aina toa mifano **miwili.** (alama 5)

(i) Vipasuo

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(ii) Vipasuo-kwamizo

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(iii) Kitambaza

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(iv) Kimadende

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(v) Nazali

..............................................................................................................

..............................................................................................................

2)

(a) Nini maana ya silabi? (alama 2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(b) Huku ukitumia mifano, onyesha miundo **mitatu** ya silabi za Kiswahili. (alama 3)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(c) Fafanua istilahi zifuatazo: (alama 4)

(i) Kiimbo:..............................................................................................................

..............................................................................................................

(ii) Shadda:..............................................................................................................

..............................................................................................................



for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call:0720502479

(d) Tambua aina za maneno yaliyotumika kwenye sentensi zifuatazo. (alama 5)

(i) Fatuma na watoto wawili watasafiri.

(ii) Akal Mwalimu mrefu anaandika vizuri.

(e) Kamilisha methali hizi: (alama 4)

(i) Mwenda pole ..........................................................................................

(ii) Angaruka juu kipungu ...............................................................................

(iii) Msafiri ni ....................................................................................................

(iv) Polepole ya Kobe ......................................................................................

(f) Onyesha viambishi awali na tamati katika sentenzi hizi: (alama 4)

(i) Anawakimbilia

(ii) Palipendekeza

(g) Akifisha sentensi hii ipasavyo. (alama 3)

Mwalimu alimwambia okireng'ende aende kitale kasha nairobi.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(h) Huku ukitoa mifano eleza aina zozote **nne** za Nomino. (alama 8)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

3. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Sajili ni nini? (alama 2)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

(b) Fafanua sifa **nne** za sajili ya biashara. (alama 8)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

4. **FASIHI (ALAMA 10)**

(a) (i) Chemsha bongo ni nini? (alama 2)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

(ii) Eleza dhima zozote **tatu** za maigizo. (alama 3)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

(b) (i) Ni nini maana ya hadithi fupi? (alama 2)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

(ii) Taja tamathali zozote **tatu** zinazotumika katika riwaya. (alama 3)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479